**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**

---

**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MIUNDOMBINU**

# TAARIFA KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI KWA MWAKA WA FEDHA WA 2021/2022; PAMOJA NA MAONI NA USHAURI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA HIYO KWA MWAKA WA FEDHA WA 2022/2023

---

*[Inatolewa Chini ya Kanuni ya 118 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020]*

23 Mei, 2022

## VIFUPISHO

| | |
|---|---|
| PPP | Public Private Partnership |
| CSR | Corporate Social Responsibility |
| TAA | Tanzania Airports Authority |
| TCAA | Tanzania Civil Aviation Authority |
| ATCL | Air Tanzania Company Limited |
| TEMESA | Tanzania Electronical Mechanical and Electronics Services Agency |
| TMA | Tanzania Meteorological Authority |
| TAZARA | Tanzania and Zambia Railway Co. |
| TANROADS | Tanzania National Roads Agency |
| TASAC | Tanzania shipping Agencies Corporation |
| LATRA | Tanzania Transport Regulatory Authority |
| TPA | Tanzania Ports Authority |
| MSCL | Marine Services Company Limited |

# TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MIUNDOMBINU KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI KWA MWAKA WA FEDHA WA 2021/2022; PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA HIYO KWA MWAKA WA FEDHA WA 2022/2023

## SEHEMU YA KWANZA

### 1.0 Utangulizi

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa **Kanuni ya 118 (9)** ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni 2020, naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu Kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Sekta ya Ujenzi **fungu 98)** Sekta ya Uchukuzi **fungu 62)** kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 pamoja na Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

**Mheshimiwa Spika,** majukumu ya Kamati kuhusiana na Uchambuzi wa Bajeti ya kila mwaka ya Wizara inazozisimamia yameelekezwa katika Fasili ya 7(1)(a) ya nyongeza ya Nane ya Kanuni za kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020.

**Mheshimiwa Spika,** katika kutekeleza jukumu hili, Kamati ilikagua baadhi ya miradi iliyotengewa fedha katika Mwaka wa Fedha 2021/2022 na pia ilichambua taarifa za utekelezaji wa bajeti ya Wizara kwa mwaka huo.

## 1.1 Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo Iliyotengewa Fedha

**Mheshimiwa Spika,** kamati ilifanya ziara ya ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo inayotekelezwa chini ya Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi. Ziara hizo zilifanyika kati ya tarehe 13 hadi 21 Machi 2022 Kanda ya Ziwa katika Mkoa wa Mwanza na Kagera.

Jumla ya miradi iliyotembelewa na kukaguliwa na Kamati katika Sekta ya Ujenzi ni mitatu nayo ni:-

a) Mradi wa ujenzi na ukarabati wa vivuko, Maegesho na karakana unaotekelezwa na TEMESA;

b) Mradi wa ujenzi wa Miundombinu ya Viwanja vya Ndege; na

c) Mradi wa Ujenzi wa Barabara na Madaraja;

**Mheshimiwa Spika,** aidha, Kamati ilitembelea miradi mingine mitatu (3) katika sekta ya Uchukuzi kama ifuatavyo:-

a) Mradi wa ujenzi wa reli ya kisasa (SGR) kipande cha Mwanza – Isaka (Mradi Na. 4282);

b) Mradi wa ununuzi wa Rada, vifaa na ujenzi wa miundombinu ya hali ya hewa – Mwanza (Mradi Na. 4290); na

c) Mradi wa ujenzi na ukarabati wa Meli kwenye Maziwa Makuu – Ziwa Victoria (Mradi Na. 4295).

## 1.2 Matokeo ya Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo

### a) Miradi ya Sekta ya Ujenzi

#### 1.2.1 Mradi wa ujenzi na Ukarabati wa Vivuko, Maegesho na Karakana unaotekelezwa na TEMESA;

**Mheshimiwa Spika,** tarehe 13 -14 Machi, 2022, Kamati ilitembelea mradi wa ujenzi na ukarabati wa vivuko, maegesho na karakana unaotekelezwa na TEMESA;

**Mheshimiwa Spika,** mradi huu jumla ulitengewa **Sh. 84,913,214,000** kwa mwaka 2021/2022, kwa mchanganuo ufuatao:-

- **Ujenzi na Ukarabati wa Vivuko na Maegesho**

  **Mheshimiwa Spika**, Wizara kupitia Wakala wa Ufundi na Umeme Tanzania (TEMESA) ilitengewa jumla ya **Sh. 3,046,830,000** kutekeleza mradi huu. Ilipanga kukamilisha upanuzi wa eneo la maegesho ya Kigamboni katika kivuko cha Magogoni na ujenzi wa vivuko vya miundombinu ya vituo kumi na kivuko cha Kisorya. Aidha, Wizara ilipanga kufanya ukarabati wa vivuko vya MV Musoma, MV Mara, MV Ujenzi, MV Kome II, MV Misungwi, MV Nyerere, MV Mafanikio, MV Kyanyabasa, MV Tanga na Vivuko vingine kama ilivyoainishwa kwenye taarifa ya Wizara.

**Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia Machi, 2022 Wakala umesimamia na kuendesha vivuko 33 na boti saba katika vituo 22 nchini. Ujenzi wa upanuzi wa jengo la abiria katika maegesho ya Magogoni- Kigamboni, maegesho ya kipande cha Nyamisati, kivuko cha MV Mafanikio umekamilika. Pia inaendelea kutekeleza ujenzi wa vivuko vya miundombinu ya vituo kumi, ujenzi wa kivuko kipya cha Kisorya – Rugezi, vivuko vingine vya Ijinga – Kahangala, Bwiro – Bukondo, Nyakarilo – Kome na kivuko cha pili cha Nyamisati – Mafia.

- **Miradi ya Nyumba na Majengo ya Serikali**
  **Mheshimiwa Spika,**

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2021/2022, Wizara ilitengewa **Sh. 69,601,084,000** kwa ajili ya ujenzi wa nyumba (20) za viongozi, watumishi wa umma, ukarabati wa nyumba za Serikali, ujenzi wa nyumba za Waheshimiwa Majaji katika mikoa 5, ujenzi wa nyumba za makazi Ikulu Dodoma, ujenzi wa nyumba za makazi 150 za watumishi wa Umma katika Jiji la Dodoma na miradi mingine kama ilivyoonesha kwenye randama.

**Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia Januari, 2022, utekelezaji wa miradi uko katika hatua mbalimbali kama ifuatazo;

i) Ujenzi wa nyumba 20 za viongozi asilimia **90**

ii) Ukarabati wa nyumba za viongozi jijini Dodoma asilimia **35;**

iii) Ujenzi wa nyumba 5 za Majaji Tanzania Bara upo katika hatua mbalimbali za utekelezaji;

iv) Ujenzi wa nyumba za makazi 150 za watumishi wa umma katika Jiji la Dodoma, asilimia **70**; na

- **Ujenzi na Ukarabati wa Karakana**

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2021/2022, Wizara ilipanga kufanya ukarabati wa Karakana kumi na moja (11) zilizopo Mwanza, Arusha, Mtwara, Mbeya, M.T Depot Dar es Salaam, Tabora, Kigoma, Mara, Ruvuma, Pwani na Vingunguti, ujenzi wa Karakana mpya ya Kisasa Jijini Dodoma, ununuzi wa karakana zinazotembea sita (6), uanzishaji wa karakana za Wilaya ya Same, Simanjiro, Masasi, Ukerewe, Chato na Kyela  na ujenzi wa karakana za TEMESA katika mikoa mipya mitano (5) na miradi mingine kama iliyowasilishwa na mtoa hoja

**Mheshimiwa Spika,** hadi Januari, 2022, ukarabati wa karakana ya TEMESA Wilaya ya Same, TBA

Dodoma, Mbeya, M.T Depot – Dar es salaam, Pwani, Vingunguti na Simiyu awamu ya kwanza umekamilika.

### 1.2.2 Miradi ya Ujenzi wa Barabara na Madaraja

**Mheshimiwa Spika, lengo la mradi huu ni kujenga,** kukarabati na kufanyia matengenezo barabara kuu na za mikoa zenye jumla ya kilometa **36,258.** Katika mwaka wa fedha wa 2021/2022, Wizara ilitengewa **Sh. 1,406,271,340,000** kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya barabara na madaraja. Kati ya fedha hizo fedha za ndani ni **Sh. 1,137,418,670,000** na **Sh. 268,852,680,000** ni fedha za nje. Fedha za ndani zilijumlisha fedha za Mfuko Mkuu wa Serikali **Sh. 501,569,540,000,** na fedha za Mfuko wa Barabara **Sh. 635,849,130,000.**

**Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka 2021/2022 TANROADS ilipanga kujenga barabara kuu zenye urefu wa kilometa **467.11** kwa kiwango cha lami ikiwa ni pamoja na ukarabati wa kilometa **32.47**, kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa miradi 63 ya barabara kuu, ujenzi wa barabara na miundombinu ya Mabasi yaendayo Haraka awamu ya pili, tatu na nne na barabara za mchepuo katika mikoa ya Mbeya, Mwanza, Iringa na Dodoma.

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa barabara za mikoa, ilipanga kujenga na kukarabati kwa kiwango cha lami barabara zenye urefu wa kilometa **103** ambapo kilometa **72.20** zilipangwa kujengwa kwa kutumia fedha za Mfuko Mkuu wa Serikali na kilometa **30.80** zilipangwa kukarabatiwa kwa kutumia fedha za Mfuko wa Barabara. Aidha, kilometa **1124.3** zilipangwa kukarabatiwa kwa kiwango cha changarawe. Ujenzi wa madaraja makubwa 14 unaendelea kama vile Kigongo – Busisi, daraja la Kitengule, daraja la Gerezani na mengine kama yalivyoainishwa katika taarifa ya Wizara.

**Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia Januari, 2022 kwa upande wa barabara kuu, ujenzi kwa kiwango cha lami umefikia asilimia **41.53** ya lengo la mwaka 2021/2022 ambapo jumla ya kilometa **193.99** zimekamilika na jumla ya kilometa **2.5** kwa kiwango cha lami zimekarabatiwa, sawa na asilimia **7.7.** Aidha, upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa miradi 20 umekamilika na miradi mingine 43 ipo katika hatua mbalimbali ya utekelezaji.

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa utekelezaji wa barabara za Mikoa, jumla ya kilometa **6.55** kati ya kilometa **103.** sawa na asilimia **6.36** zimejengwa kwa

kiwango cha lami. Aidha, kilometa 84.08 kati ya kilometa **1,124.20** sawa na asilimia **7.5** ya lengo la mwaka zilifanyiwa ukarabati kwa kiwango cha changarawe. Vilevile ujenzi wa madaraja makubwa manne (4) ulikuwa umekamilika na madaraja makubwa 10 yapo kwenye hatua mbalimbali za utekelezaji.

**Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia Januari, 2022 Wizara kupitia TANROADS imetekeleza miradi mikubwa ya madaraja kama vile daraja jipya la Wami (Pwani) utekelezaji umefikia **asilimia 72.88,** ujenzi wa barabara ya mzunguko wa nje Dodoma km **112.3.** Ujenzi wa barabara ya mzunguko wa ndani Dodoma km 15.0, ujenzi wa barabara ya mzunguko wa kati Dodoma **km 47,** Daraja la Kigongo – Busisi (Mwanza) umefikia asilimia **36.94**, Daraja jipya la Tanzanite km **1.0300,** ujenzi wa barabara ya Tabora – Ipole – Koga – Mpanda km **365.98** barabara ya Kidahwe-Kasulu-Kibondo-Nyakanazi (**km 341.25)** umekamilika.

Miundombinu ya mabasi yaendayo kasi awamu ya pili (km 20.3) umefikia asilimia **47.30**; awamu ya tatu (23.6) na nne (km 25.9) na upanuzi wa barabara ya Kimara - Kibaha kuwa njia nane km **19.2** umefikia asilimia **80.50.**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imebaini mambo yafuatayo katika miradi hii:-

i) Utekelezaji wa miradi ya barabara kuu, barabara za mikoa na ujenzi wa madaraja uko chini ya malengo.Kamati inaona kuwa hali hii hairidhishi; na

ii) Ucheleweshaji wa kutoa msamaha wa kodi ya ongezeko la thaman (VAT) unachangia kuchelewesha utekelezaji wa miradi.

**Kamati inashauri Serikali kuongeza fedha kwenye miradi ya barabara.**

### 1.2.3 Miradi ya Kujengewa Uwezo

**Mheshimiwa Spika,** lengo la mradi huu ni kujenga uwezo wa Watumishi wa Sekta ya Ujenzi kwa kuwapatia mafunzo kwa lengo la kuwaimarisha kitaaluma na kuwajengea uzoefu wa kazi. Kwa mwaka 2021/2022 mradi huu ulitengewa **Sh.318,680,000.00**, Wizara ilipanga kuwapatia mafunzo watumishi na ununuzi wa vifaa na magari.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imejulishwa kuwa matokeo ya ufuatiliaji huo yameonyesha kupungua kwa idadi ya magari yanayozidisha uzito, mfano, kiwango cha uzidishaji uzito katika magari kimepungua kutoka asilimia **0.77** kwa mwaka wa fedha 2019/2020 hadi kufikia asilimia **0.61** kwa mwaka wa fedha 2021/2022. Aidha,

Watumishi 600 wa Wizara (Ujenzi) na Taasisi zake wamehudhuria mafunzo

**b) Miradi ya Sekta ya Uchukuzi**

### 1.2.4 Mradi wa Ujenzi wa Reli ya Kisasa (SGR) – Mradi Na. 4282

**Mheshimiwa Spika,** mradi ulitengewa bajeti ya **Sh. Bilioni 897.00** hadi kufikia februari 2022 sh. **Trilioni 1.173** utekelezaji wa mradi huu umefikia hatua zifuatavyo:- taarifa za Wizara zimeonesha kuwa hadi Kamati ilipokagua na kuchambua taarifa za utekelezaji mradi huu umefikia hatua mbalimbali kwa mfano, ujenzi wa reli ya SGR kutoka Dar Es Salaam – Morogoro (Km 300) umefikia **asilimia 95,** kipande cha kutoka Morogoro – Makutupora (Km 422) kimefikia **asilimia 82.68,** kipande cha Mwanza – Isaka (Km 341) umefikia **asilimia 4.98** ya lengo. Aidha, ujenzi wa kipande cha Makutopora – Tabora (Km 368) Mkandarasi yupo kwenye hatua za mwisho za maandalizi kabla ya kuanza ujenzi. Kwa taarifa hiyo kamati imebaini yafuatayo:-

i) Kasi ya utekelezaji wa mradi huu ni ya kuridhisha kwani upatikanaji wa fedha za utekelezaji wa mradi hadi mwezi Februari, 2022 ni wa kuridhisha. Kiasi cha fedha kilichopatikana ni sawa na **asilimia 131** ya bajeti

iliyoidhinishwa na Bunge kwa kipindi cha robo tatu ya muda wa utekelezaji;

ii) Kuchelewa kufika kwa mabehewa ya treni ikilinganishwa na lengo lililowekwa kwa mwaka wa fedha 2021/2022 ambapo ulitarajiwa kukamilika Februari, 2022. Mkandarasi amechelewa kutokana na changamoto ya *Uviko 19*. Hata hivyo, Kamati imejulishwa kuwa, Mkandarasi ataleta vifaa hivyo kwa awamu tatu na atakamilisha ifikapo Septemba, 2022; na

iii) Kuchelewa kukamilika kwa kipande cha kutoka Dar Es Salaam – Morogoro ikilinganishwa na lengo lililowekwa kwa mwaka wa fedha 2021/2022 ambapo ulitarajiwa kukamilika Agosti, 2021. Hata hivyo Kamati ilijulishwa kuwa reli ya kisasa kipande cha Dar Es Salaam-Morogoro ilitarajia kuanza kufanyiwa majaribio mwezi Mei, 2022.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilibaini kuwa kuna mahitaji makubwa ya fedha kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huu. Aidha, kiasi kilichotumika mpaka sasa ni zaidi ya fedha zilizotengewa kwa mwaka 2021/2022. Kamati inaipongeza Serikali kwa jitihada za kutafuta fedha zaidi kwa lengo la kukamilisha ujenzi wa reli hii muhimu kwa maendeleo ya nchi na wananchi.

### 1.2.5 Mradi wa Ununuzi wa Rada, Vifaa na Ujenzi wa Miundombinu ya Hali ya Hewa – Mradi Na. 4290

**Mheshimiwa Spika,** mradi huu ulilenga kuboresha utabiri wa hali ya hewa nchini kwa kununua Rada saba (7) na vifaa vya hali ya hewa pamoja na ujenzi wa miundombinu.

**Mheshimiwa Spika,** matokeo ya ukaguzi na uchambuzi wa taarifa yanabainisha kuwa, hadi kufikia mwezi Februari, 2022, mradi ulipata fedha kiasi cha **asilimia 20.9** ya lengo**.** Hali hii inaonesha kuwa upatikanaji wa fedha kwa mradi huu sio wa kuridhisha. Aidha, kuna uhitaji mkubwa wa fedha katika kutekeleza mradi huu ambapo pindi utakapokamilika utaimarisha Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania.

### 1.2.6 Mradi wa Ujenzi na Ukarabati wa Meli kwenye Maziwa Makuu - Mradi Na. 4295

**Mheshimiwa Spika**, mradi huu ulilenga kuboresha usafiri wa abiria na mizigo katika Maziwa Makuu ya Victoria, Tanganyika na Nyasa. Aidha, Kamati ilibaini kuwa upatikanaji wa fedha kwa ajili ya mradi umekuwa hauridhishi kama ilivyopangwa kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

**Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia mwezi Februari, 2022, mradi ulipata fedha kiasi cha asilimia **9.8** ya lengo. Hali

hii inaonesha kuwa upatikanaji wa fedha kwa mradi huu sio wa kuridhisha.

**Mheshimiwa Spika**, meli zinazoendelea na ujenzi na ukarabati ni MV Mwanza Hapa Kazi Tu, MV Umoja na MV Sangara imefikia hatua ya asilimia **60**, asilimia **23.30** na asilimia **18.14** mtawalia**.**

### 1.2.7 Mradi wa Ununuzi wa Ndege

**Mheshimiwa Spika**, kusudio la mradi huu ni ufufuaji wa Kampuni ya Ndege Tanzania (ATCL) ili iweze kutoa huduma za usafiri wa anga ndani na nje ya nchi.

**Mheshimiwa Spika**, hadi Februari, 2022, kampuni imeweza kurejesha safari katika kituo cha Mtwara na kuanza safari kutoka Dar es Salaam kwenda Mwanza kupitia Dodoma. Hivyo basi, ATCL inatoa huduma katika vituo 15 ndani ya nchi. Hali hii inaonesha kuendelea kukua kwa kampuni. Kamati inaipongeza Serikali kwa jitihada za dhati inazofanya katika kufufua kampuni hii na imeonesha dhamira njema kwani, imefanya ununuzi wa ndege tano (5) za abiria na mizigo.

**Mheshimiwa Spika**, kusudio la mradi huu ni ufufuaji wa Kampuni ya Ndege Tanzania (ATCL) ili iweze kutoa huduma za usafiri wa anga ndani na nje ya nchi hadi Februari, 2022, kampuni imeweza kurejesha safari katika kituo cha Mtwara na kuanza safari kutoka Dar es

Salaam kwenda Mwanza kupitia Dodoma. Hivyo basi, ATCL inatoa huduma katika vituo 15 ndani ya nchi. Hali hii inaonesha kuendelea kukua kwa kampuni.

**Kamati inaipongeza Serikali kwa jitihada ya kufufua kampuni hii kwa kuongeza ununuzi wa ndege tano (5) za abiria na mizigo.**

### 1.2.8 Mradi waUjenzi wa Viwanja vya Ndege

**Ujenzi wa Uzio wa Kiwanja cha Ndege cha Mwanza**

**Mheshimiwa Spika**, Ujenzi wa uzio wa Kiwanja cha Ndege cha Mwanza umekamilika na uboreshaji wa Kiwanja cha Arusha umefikia asilimia **10.**

## 1.3 Maoni ya Jumla kuhusu Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo iliyotembelewa na Kamati

a) **Miradi ya barabara na madaraja**

i) Fedha za bajeti iliyoidhinishwa mwaka 2021/2022 zilitumika kulipa madeni badala ya kutekeleza miradi iliyokusudiwa;
ii) Kutokuwepo kwa mpango unaoruhusu ujenzi wa barabara kwa ubia (PPP);
iii) Uharibifu wa barabara na madaraja kipindi cha mvua;
iv) Kutokuwepo kwa bajeti ya ukarabati wa barabara zilizopandishwa hadhi;
v) Athari za mikataba kwa Wakandarasi kwa kuchelewa kulipwa madeni;

vi) Changamoto ya vitendea kazi na maslahi ya watumishi katika miradi;
vii) Wakandarasi kushindwa kutoa fedha za (CSR) kwa jamii zilizopo karibu na mradi.
viii) Kuna Changamoto ya ulinzi na utunzaji wa mazingira katika madaraja; na
ix) Wadau wanaochangia miradi watambuliwe.

b) **Ujenzi na Ukarabati wa Vivuko, Maegesho na Karakana**

i) Ujenzi na ukarabati wa Kararakana na Vivuko hauridhishi;
ii) Uchakavu mkubwa wa vivuko vilivyotumika kwa zaidi ya miaka 50;
iii) Kukosekana kwa Msimamizi na Mkaguzi katika miradi ya TEMESA ni changamoto kubwa. Aidha kuna uhaba wa gereji na vipuri vya magari;
iv) Kushindwa kuacha kiasi cha fedha za makusanyo kwa ajili ya uendeshaji na ukarabati wa vivuko;
v) Kuna Changamoto ya kutegemea mkandarasi mmoja katika kutengeneza vivuko; na
vi) Kutokushirikishwa kwa Kampuni binafsi katika kutoa huduma ya vivuko nchini.

c) **Ujenzi na Ukarabati wa Meli za MSCL**

i) Kutokamilika kwa wakati kwa ujenzi wa meli na kukosa usimamizi;

ii) Kukosekana kwa fedha za mishahara;
iii) Kutoshirikishwa kwa ukaribu kwa wazawa katika ulinzi na utekelezaji wa miradi;
iv) Uchakavu wa miundombinu ya Bandari;
v) Kutotekelezwa kwa ahadi za Serikali;
vi) Upungufu wa meli ziwa nyasa;
vii) Kushirikiana kwa TPA na TRC katika kusafirisha mizigo; na
viii) Uchakavu wa meli zinazotoa huduma kwa zaidi ya miaka 50.

d) **ATCL, TAA na TCAA**
i) Mzigo wa madeni kwa mashirika ya ATCL, TAA na TCAA;
ii) Gharama kubwa za usafiri wa ndege ndani ya nchi;
iii) Changamoto ya ujenzi wa vya Viwanja vya Ndege kutokutekelezwa na TAA; na
iv) Kukosekana kwa ndege kubwa kwenda Dar es Salaam – Dodoma na uwepo wa Mawakala wanaohujumu ATCL.

e) **Mamlaka ya udhibiti , Usafiri Ardhini (LATRA)**
i) Madereva kuendesha mwendokasi zaidi ya km 80 kwa saa.

f) **Mamlaka ya Reli ya Tanzania na Zambia (TAZARA)**
i) Mashine ya kuponda kokoto TAZARA Mbeya kushindwa kuonesha ufanisi; na

ii) Uchakavu wa Mabehewa ya TAZARA.

g) **Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania – TMA**

i) Kutoboreshwa kwa maslahi ya Watumishi; na

ii) Kuna changamoto ya Mamlaka kutolipwa madeni yake kwa wakati.

## SEHEMU YA PILI

## 2.0 UCHAMBUZI WA BAJETI

### 2.1 UCHAMBUZI WA UTEKELEZAJI WA BAJETI PAMOJA NA MAONI, USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022

**Mheshimiwa Spika,** Uchambuzi wa Kamati kuhusu utekelezaji wa Bajeti na Majukumu ya Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi Sekta ya Ujenzi (Fungu 98) na Sekta ya Uchukuzi (Fungu 62) kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 ulijikita katika maeneo makuu manne (4) ambayo ni:-

a) Utekelezaji wa Vipaumbele vya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022;

b) Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 kuhusu ukusanyaji wa Maduhuli;

c) Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 kuhusu upatikanaji wa fedha; na

d) Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo yaliyotolewa na Kamati kwa Bajeti ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.

### 2.1.1 Uchambuzi wa Utekelezaji wa Vipaumbele vya Wizara

**Mheshimiwa Spika,** katika kufanya uchambuzi katika Wizara hii, Kamati imezingatia mambo mbalimbali kama vile Mpango wa Taifa wa Tatu wa Maendeleo wa Miaka Mitano 2021/2022 - 2025/2026, Ilani ya Uchaguzi Mkuu ya CCM ya Mwaka 2020 – 2025 na Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs Lengo na. 9) inasisitiza masuala ya viwanda ubunifu na miundombinu. Wizara ina vipaumbele vilivyozingatiwa katika mgawanyo wa fedha za kutekeleza Miradi ya Maendeleo kwa mwaka wa fedha 2022/23 ni kukamilisha miradi inayoendelea pamoja na kutekelea miradi mipya kama ifuatavyo: -

i) Miradi iliyoanishwa kwenye Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2020;

ii) Miradi iliyoanishwa kwenye Mpango wa Tatu wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2021/22 – 2025/26);

iii) Miradi iliyo kwenye ahadi mbalimbali za Viongozi wa Serikali;

iv) Miradi ambayo Washirika wa Maendeleo wameonesha nia ya kutoa fedha za utekelezaji ambapo Serikali inawajibika kutoa mchango wake (Counterpart Fund);

v) Miradi ya Kimkakati inayohusu barabara, madaraja, viwanja vya ndege na vivuko (kama vile ulinzi wa mipakani pamoja na barabara zinazoingia na kutoka kwenye maeneo ya kimkakati);

vi) Miradi ya barabara zinazokwenda kwenye vituo vya Reli ya Kisasa (Standard Gauge Railway – SGR); na

vii) Miradi ya barabara ambayo imekuwa ikipendekezwa na Bodi za Barabara za Mikoa.

### 2.1.2 Uchambuzi wa Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka 2021/2022 kuhusu ukusanyaji wa Maduhuli

**Mheshimiwa Spika**, wakati wa Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi, Kamati ilichambua Makadirio ya Maduhuli kwa mwaka wa fedha 2022/2023, ikilinganisha na 2021/2022.

**Jedwali Na. 01 linalohusu makusanyo ya Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi**

| Sekta | Makadirio ya Makusanyo kwa mwaka 2021/2022 | Makusanyo hadi kufikia Februari 2022 | Asilimia | Makadirio Makusanyo mwaka 2022/23 | % Ongezeko |
|---|---|---|---|---|---|
| Ujenzi | 70,000,000 | 49,170,000 | 70.24 | 70,000,000 | 0 |
| Uchukuzi | 1,887,072,747,303. | 1,109,005,289, | 58.77 | 2,087,927,769,199 | 10.64 |

**Chanzo:** Randama ya Wizara

### i) Makusanyo ya Maduhuli Sekta ya Ujenzi

**Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2021/2022, Sekta ya Ujenzi (Fungu 98) ilipaswa kukusanya jumla ya **Sh. 70,000,000** kutoka Idara ya Utawala na Rasilimali Watu na Huduma za Ufundi. Taarifa zilionesha kuwa hadi kufikia Mwezi Januari, 2022 kiasi

kilichokusanywa ni **Sh. 49,170,000** sawa na **asilimia 70.24** ya lengo la jumla la makusanyo kwa Sekta ya Ujenzi. Makusanyo hayo yamepatikana ndani ya robo tatu (yaani asilimia 75) za kipindi cha utekelezaji wa majukumu. Hali hiyo ni ishara nzuri ya kufikia lengo lililowekwa kwani bado **asilimia 29.76** kufika lengo.

**ii) Makusanyo Sekta ya Uchukuzi**

**Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2021/2022, Sekta ya Uchukuzi (fungu 62) kupitia taasisi zake, zilipaswa kukusanya jumla ya **Sh. 1,887,072,747,303.**

Taarifa zilionesha kuwa hadi kufikia mwezi Februari, 2022, kiasi kilichokusanywa ni **Sh. 1,109,005,289,621** sawa na **asilimia 58.77** ya lengo la jumla la makusanyo. Makusanyo hayo yamepatikana ndani ya robo tatu. Hali hiyo ni ishara ya kutofikiwa lengo lililowekwa katika muda uliobaki wa kumaliza mwaka wa fedha.

**Mheshimiwa Spika,** kiujumla makusanyo ya mapato kwa taasisi ni wakuridhisha isipokuwa Chuo cha DMI, Chuo cha NIT, TMA na TCAA.

**Mheshimiwa Spika**, **Kamati ina maoni kuwa malengo yaliyowekwa yazingatiwe katika ukusanyaji wa mapato.**

### 2.1.3 Uchambuzi wa Upatikanaji wa Fedha kufikia Februari, 2022

**a) Sekta ya Ujenzi**

**Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka wa fedha wa 2021/2022 Sekta hii pamoja na Taasisi zake kwa pamoja walitengewa jumla ya **Sh. 38,540,786,999.96** kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Kati ya

fedha hizo **Sh. 35,186,389,000** ni mishahara ya watumishi na **Sh. 3,354,398,000** kwa ajili ya matumizi mengineyo.

**Mheshimiwa Spika**, hadi mwezi Februari, 2022 jumla ya **Sh. 19,475,506,891** sawa na **asilimia 51** zilipatikana. **Sh 17,310,203,948** ni mishahara na **Sh.2,165,302,943** za matumizi mengineyo.

**b) Sekta ya Uchukuzi**

**Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka wa fedha wa 2021/2022 Sekta hii pamoja na taasisi zake kwa pamoja walitengewa jumla ya ya **Sh.91,957,583,468** kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Hadi mwezi Februari, 2022 jumla ya **Sh. 56,563,730,422.86** sawa na asilimia **61.51** zilipatikana.

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi umeonesha kwamba, fedha zilizopokewa kwa ajili ya matumizi ya uendeshaji (OC) ya Sekta na taasisi zake ni **Bilioni 27.07** sawa na **asilimia 47.86** kwa kiasi hicho cha fedha inaonyesha kuwa kuna upungufu wa fedha za uendeshaji.

### 2.1.4 Uchambuzi wa Utekelezaji wa Maoni na Ushauri uliotolewa na Kamati kwa mwaka 2021/2022

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilitoa maoni kwa maeneo ambayo bado hayajatekelezwa kikamilifu au utekelezaji wake unaendelea.

Kamati itayasisitiza katika taarifa hii likiwemo suala la kufanya marekebisho kwa sheria ya reli ya TAZARA ili nchi yetu iweze

kunufaika na reli hiyo, na Jamii iliyopo eneo la mradi ikumbukwe kwa kujengewa huduma za kijamii (CSR);

## 2.2 Uchambuzi wa Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Fungu 98 & Fungu 62) kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilifanya uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi kwa sekta ya Ujenzi **Fungu 98** na sekta ya Uchukuzi **Fungu 62** kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023, na kufanya ulinganisho kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa Mwaka (2021/2022) . Mambo yafuatayo yalizingatiwa:-

a) Malengo ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023;
b) Makadirio ya Makusanyo ya Maduhuli kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023;
c) Makadirio ya Matumizi Mwaka wa Fedha 2022/2023;
d) Bajeti ya Wizara dhidi ya Bajeti ya Taifa; na
e) Mambo ya Ujumla katika Sekta ya Ujenzi na Uchukuzi.

### 2.2.1 Uchambuzi wa malengo ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023

**Mheshimiwa Spika**, kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023, Kamati ilichambua na kufanya ulinganisho kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha (2021/2022). Maeneo yaliyofanyiwa Uchambuzi ni kama ifuatavyo:-

i) Malengo ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023;

ii) Makadirio ya Makusanyo ya Maduhuli kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023; na

iii) Makadirio ya Matumizi Mwaka wa Fedha 2022/2023.

### 2.2.2 Uchambuzi wa Makadirio ya Makusanyo ya Maduhuli kwa baadhi ya Taasisi kwa mwaka 2022/2023

**Jedwali Na. 02: Mchanganuo wa Lengo la Mapato**

| SEKTA | LENGO KWA MWAKA 2021/2022 | UKUSANYAJI HADI FEBRUARI, 2022 | % LENGO | Bajeti kwa mwaka 2022/2023 | % (+/-) kwa 2022/23 |
|---|---|---|---|---|---|
| UJENZI NA TAASISI | 1,627,244,274,199.96 | 1,113,135,342,451.16 | 68.41 | 1,465,835,235,800 | -10 |
| UCHUKUZI NA TAASISI | 1,877,841,464,245 | 1,109,005,289,621 | 59 | 2,087,927,769,199 | +11 |

**Chanzo:- Randama ya Wizara**

#### a) Sekta ya Ujenzi

**Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2022/23, Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Fungu 98-Ujenzi) inatarajia kukusanya jumla ya **Sh. 70,000,000.00** kutoka Idara zenye vyanzo vya mapato.

#### b) Sekta ya Uchukuzi

i) Katika mwaka wa fedha 2022/2023, kwa upande wa TRC, TMA, KADCO, NIT na DMI, Kamati inaona malengo waliyojiwekea yanaweza yasitimie kwani lazima yaendane na uhalisia uliopo sasa kwani hadi Februari, 2022 makusanyo yao yalikuwa chini ya asilimia **50** ya lengo kwa mwaka

2021/2022, TRC asilimia **49.09**, NIT asilimia **46.07**, DMI asilimia **46.66,** TMA asilimia **28.46.**

ii) Kwa mwaka wa fedha 2021/2022 Wizara iliweka lengo ambalo hadi kufikia mwezi Februari, 2022, lilifikiwa kwa **asilimia 59**. Hata hivyo, Kamati ilibaini kuwa, lengo la makusanyo kwa MSCL, ATCL, na TAA yameongezeka kwa asilimia **73, 21** na **25** mtawalia. Hali hiyo inaweza kutafsiriwa kuwa, vyanzo vya mapato kwa MSCL, ATCL na TAA vimeongezeka au kuna matarajio ya kuimarisha ukusanyaji wa mapato; na

iii) **Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa TAZARA, LATRA, TASAC, TPA, na SINOTASHIP, Kamati imebaini kuwa mwaka 2021/2022 taasisi hizi zilifanya vizuri katika makusanyo na malengo yaliyowekwa yanaakisi uzingatiwaji wa uzoefu wa makusanyo kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

### 2.2.3 Uchambuzi wa Makadirio ya Matumizi kwa mwaka wa fedha 2022/2023-

i) **Matumizi ya Jumla Sekta ya Ujenzi (Fungu 98)**

**Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka wa fedha wa 2022/2023, Bunge lako tukufu linaombwa kuidhinisha Matumizi ya Kawaida kwa sekta ya Ujenzi na taasisi zake jumla ya **Sh. 44,293,050,000.00** sawa ongezeko la **asilimia 14.93**

ukilinganisha na mwaka **2021/2022.** Kati ya fedha Matumizi ya Mishahara kwa watumishi wa Wizara na taasisi zake ni **Sh. 40,638,652,000.00** sawa na **asilimia 15.50** na Matumizi Mengineyo **Sh. 3,654,398,000.00** sawa na ongezeko la **asilimia 8.94** ikilinganishwa na mwaka 2021/2022.

Aidha, inaomba kuidhinishiwa **Sh.1,421,542,185,800.00** kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo. Bajeti hii imepunjwa kwa **asilimia 10.52** ukilinganisha na mwaka 2021/2022. Kati ya fedha hizo, **Sh. 1,168,576,368,800.00** ni fedha za ndani na **Sh. 252,965,817,000.00** ni fedha za nje. Aidha**, Sh. 599,756,467,800.00** kati ya fedha za ndani ni fedha za Mfuko wa Barabara.

**Mheshimiwa Spika,** kwenye Sekta ya Ujenzi uchanganuzi uliofanyika, Kamati inabainisha yafuatayo:-

**a)** Kuna upungufu wa fedha za maendeleo kwa **Sh. 167,161,301,400.00 sawa na asilimia 10.52** ukilinganisha na mwaka 2021/2022,

**b)** Upungufu umeonekana kwenye mradi wa usalama barabarani na mazingira umepungua kwa **asilimia 14**, ujenzi wa miundombinu ya Viwanja vya Ndege kwa **asilimia 9.48,** miradi ya barabara imepungua kwa **asilimia 10.37,** ujenzi na ukarabati wa Vivuko, maegesho, karakana, nyumba na majengo ya Serikali imepungua kwa **asilimia 14** miradi ya kujengewa uwezo imepungua kwa **asilimia 14.** Kuna ongeko

la Matumizi ya Kawaida kwa **asilimia 14.93** kwa mwaka 2022/2023 ukilinganisha na mwaka 2021/2022;

c) Makadirio ya matumizi mengineyo (OC) kwa Taasisi zilizo chini ya Sekta ya Ujenzi kwa mwaka 2022/2023 yameongezeka kwa **asilimia 8.94** ukilinganisha na mwaka 2021/2022;

d) Makadirio ya fedha za Matumizi ya Mishahara kwa watumishi wa Sekta ya Ujenzi kwa mwaka 2022/2023 yameongezeka kwa **asilimia 15.50** ukilinganisha na mwaka 2021/2022, sababu zilizopelekea mishahara kupanda ni pamoja na Serikali kuendelea kuboresha maslahi ya watumishi; na

e) Uwezo wa Mfuko wa Barabara kugharamia matengenezo ya barabara za Kitaifa na Wilaya utapungua kwa **Sh. 35,000,000,000.00** wastani wa **asilimia 46.**

**Mheshimiwa Spika, Kamati inaendelea kusisitiza kuwa upungufu huo unaweza kukwamisha utekelezaji wa miradi ya maendeleo.**

ii) **Matumizi ya Jumla ya Sekta ya Uchukuzi (Fungu 62)**

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha wa 2022/2023, Bunge lako tukufu linaombwa kuidhinisha makadirio ya Matumizi ya Kawaida kwa Sekta ya Uchukuzi na taasisi zake jumla ya **Sh. 94,546,502,000.00** sawa ongezeko la **asilimia 3.06** ya mwaka 2021/2022. Kati ya fedha hizo

Matumizi ya Mishahara kwa watumishi wa Wizara na taasisi zake ni **Sh. 65,388,693,913.00**

Kati ya fedha hizo, **Sh. 3,192,623,000** ni kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi walioko Makao Makuu na **Sh. 62,196,071,000** ni kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi wa Taasisi na Matumizi Mengineyo ni **Sh. 28,558,510,681** Kati ya fedha za matumizi mengineyo kiasi cha **Sh. 9,364,111,802** ni kwa ajili ya Makao Makuu na **Sh. 19,194,398,966** ni kwa ajili ya Taasisi zilizo chini yake.

Aidha, kwa mwaka 2022/2023 Sekta hii inaomba kuidhinishiwa **Sh. 2,306,234,938,000.00** kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo sawa na ongezeko la **asilimia 13.7** ukilinganisha na mwaka 2021/2022. Kati ya fedha hizo **Sh. 2,192,771,622,000** ni fedha za ndani na **Sh 113,463,316,000.00** ni fedha za nje.

Katika uchambuzi kamati imebaini yafuatayo:-

a) Kuna ongezeko la fedha za bajeti kwa mwaka 2022/2023 kwa **asilimia 13.24;**

b) Kuna ongezeko la fedha za maendeleo kwa **asilimia 13.7** ukilinganisha na mwaka 2021/2022 na Matumizi ya Kawaida, kwa **asilimia 3.06**; na

c) Makadirio ya matumizi mengineyo (OC) kwa Taasisi zilizo chini ya Sekta ya Uchukuzi kwa mwaka 2022/2023 yameongezeka kutoka **Sh 3,354,397,999.96** hadi **Sh. 28,558,510,681.**

**Jedwali Na 3. Matumizi kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo Sekta ya Ujenzi na Uchukuzi kwa mwaka 2021/2022 na mwaka 2022/2023**

| **Na ya Mradi** | **Mradi** | **Bajeti kwa mwaka 2021/22** | **Bajeti kwa mwaka 2022/2023** | **%** |
|---|---|---|---|---|
| **A: Sekta ya Ujenzi** | | | | |
| 1003 | Kujengewa Uwezo | 318,680,000 | 273,746,000 | -14 |
| 2002 | Technical Services Division | 84,913,214,000 | 72,940,450,000 | -14 |
| 2005 | barabara | 1,406,271,346,200 | 1,260,441,205,800 | -10.37 |
| 6001 | Viwanja vya Ndege | 95,123,113,000 | 86,102,526,000 | -9.48 |
| 5002 | Usalama Barabarani/Mazingira | 2,077,134,000 | 1,784,258,000 | -14 |
| **JUMLA** | | **1,588,703,487,200** | **1,421,542,185,800** | **-10.52** |
| **B: Sekta ya Uchukuzi** | | | | |
| 4281 | Reli ya Kisasa - SGR | 897,000,000,000 | 1,263,000,000,000 | 40.80 |
| | Jengo la tatu la Abiria – JNIA<br>DMI | 20,000,000,000<br>1,000,000,000 | 17,300,000,000<br>1,000,000,000 | -12.86 |
| | Ununuzi wa Rada na Miundombinu – TMA | 30,000,000,000 | 20,000,000,000 | -33 |
| 4294 | Ununuzi wa Ndege | 450,000,000,000 | 468,000,000,000 | 4 |
| 4295 | Ujenzi na ukarabati wa Meli kwenye maziwa Makuu - MSCL | 135,000,000,000 | 113,706,820,000 | -15.77 |
| 4201 | Lake Victoria Maritime and Transport Project | 4,240,310,000 | 4,157,240,000 | -1.96 |
| 4213 | Fedha za miundombinu | 294,801,620,000 | 294,801,620,000 | - |

| Na ya Mradi | Mradi | Bajeti kwa mwaka 2021/22 | Bajeti kwa mwaka 2022/2023 | % |
|---|---|---|---|---|
| | ya Reli | | | |
| 4216 | TIRP II- Tanzania Intermodal Railway Project | 9,193,250,000 | - | - |
| 4309 | East Africa skills for Transormation and Regional Integration Project (EASTRIP) | 4,776,680,000 | - | - |
| 6377 | Infrastructure Development and Procurement of Training Equipment (NIT) | 500,000,000,000 | 1,770,000,000 | -99.6 |
| 4227 | Dar es Salaam Maritime Gateway Project (DMGP) | 190,983,000,000 | 100,112,820,000 | 47.58 |
| 4211 | Improvement for TAZARA | - | 13,193,170,000 | - |
| **JUMLA** | | **2,028,306,410,000** | **2,306,234,938,000** | **13.7** |

**Chanzo:** Randama ya Wizara

## SEHEMU YA TATU

## 3.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

**Mheshimiwa Spika,** kwa msingi wa maoni yaliyobainishwa awali, Kamati inatoa ushauri kama ifuatavyo:-

### 3.1 Maoni ya Jumla

**1.Sekta ya ujenzi Fungu 98**

a) Miradi mipya ya barabara kushindwa kuanza utekelezaji wake kwa mwaka 2021/2022 kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo fedha zake kutumika kulipa miradi ya nyuma; na

b) Kukosekana kwa mpango wa kushirikisha sekta binafsi katika ujenzi wa barabara.

### 3.2 Maoni ya Jumla Sekta ya Uchukuzi (fungu 62)

a) Kutokuwepo kwa mkakati wa kuwadhibiti Wakandarasi wanaoshindwa kutekeleza miradi; na

b) Sheria iliyoanzisha TAZARA inachangia kuzorotesha utendaji kazi.

### 3.3 Sekta ya Ujenzi (Fungu 98)

**3.3.1 Mheshimiwa Spika,** kuhusu miradi ya Ujenzi na Ukarabati wa Karakana, Vivuko na Maegesho kamati inashauri kwamba:-

a) Serikali kupitia TEMESA ihakikishe ukarabati wa vivuko na maegesho unafanyika kwa wakati ili visilete maafa kwa wananchi;

b) Serikali ifanye tathimini ya kina juu ya ununuzi wa Meli na Vivuko vipya na hatimaye waache kutumia vivuko vilivyotumika zaidi ya miaka 50;
c) TEMESA ijiendeshe kibiashara na izingatie thamani ya fedha, uwazi na uhalisia katika miradi wanayotekeleza;
d) Serikali iisimamie TEMESA kwa kuweka msimamizi na mkaguzi katika utekelezaji wa miradi yake inayoendelea;
e) Serikali iweke ushindani kwenye miradi ya kutengeneza vivuko na maegesho;
f) Fedha zinazopatikana kutoka kwenye vivuko zitumike kufanya matengenezo madogo madogo ya vivuko ili viwe katika hali nzuri muda wote; na
g) Serikali iruhusu vivuko vya watu binafsi kufanya kazi katika vivuko nchini ili kupunguza ya adha ya usafiri kwa wananchi.

**3.3.2 Mheshimiwa Spika, kuhusu ujenzi wa daraja la Kigongo - Busisi Kamati inashauri kwamba:-**

a) Serikali imsimamie Mkandarasi amalize ujenzi wa daraja hilo kwa muda uliopangwa;
b) TANROADS ihakikishe Mkandarasi analipwa kwa wakati ili kuzuia athari za mkataba zinazoweza kutokea;
c) Malipo kwa wafanyakazi na vitendea kazi viboreshwe kama matakwa ya OSHA yanavyoelekeza; na
d) Jamii iliyopo eneo la mradi ikumbukwe kwa kujengewa huduma za kijamii (CSR);

**3.3.3 Mheshimiwa Spika, Kuhusu Daraja la Kitengule Kamati inashauri kwamba:-**

a) TANROADS wahakikishe utunzaji wa mazingira eneo la mradi unazingatiwa kwa kupanda miti na majani ili kudhibiti mmomonyoko unaoweza kuathiri daraja;

b) Serikali ihakikishe daraja linakamilika ndani ya muda uliopangwa na Mhandisi Mshauri alipwe madai yake kwa wakati;

c) Serikali na TANROADS watambue mchango uliotolewa na Kiwanda cha Sukari cha Kagera, kwa kuwapa cheti cha kuthamini mchango wao; na

d) TANROADS kwa kushirikiana na Kiwanda cha Sukari cha Kagera kihakikishe kinaweka ulinzi kwenye daraja muda wote ili kudhibiti uharibifu wa miundombinu ya daraja.

**3.3.4 Mheshimiwa Spika, kuhusu ujenzi na ukarabati wa barabara Kamati inashauri kwamba:-**

a) Serikali ihakikishe inakamilisha ujenzi wa barabara za lami za kuunganisha mikoa na nchi jirani;

b) Ni vyema Serikali ikaja na mpango wa kutenga fedha za kujenga barabara chache kuliko kuweka barabara nyingi ambazo utekelezaji wake ni mgumu;

c) ili kurahisisha barabara nyingi kujengwa nchini kwa haraka, Kamati inashauri kuwa, Serikali ije na mpango wa kushirikisha sekta binafsi katika kujenga barabara kwa mfumo wa ubia (PPP);

d) Serikali ioneshe ioneshe kiasi cha fdha kinachokwenda kulipa madeni ya madeni ya miradi ambayo bado haijakamilika wanapoleta taarifa za Wizara kwenye uchambuzi wa bajeti;
e) Serikali iweke tozo kwenye daraja jipya la Tanzanite; na
f) Barabara zilizopandishwa hadhi na kuwa chini ya TANROADS ziongezwe upana na zifanyiwe ukarabati.

## 3.4 Sekta ya Uchukuzi (fungu 62)

**3.4.1** Mheshimiwa Spika, kuhusu ujenzi na ukarabati wa Meli za MSCL Kamati inashauri kwamba:-

a) Serikali ihakikishe mkataba wa kutengeneza meli mpya ya MV Mwanza (Hapa Kazi Tu) na MV Umoja unasimamiwa na kuhakikisha kuwa ujenzi unakamilika kwa wakati;
b) MSCL wasimamie ujenzi wa miradi ya Meli iliyopo ili itekelezwe kwa ufanisi kwani Serikali imewekeza fedha nyingi;
c) Kuhakikisha fedha inalipwa kulingana na kazi iliyofanyika ili kuepusha matatizo yanayoweza kujitokeza kwa wakandarasi kukimbia kabla ya mradi kukamilika
d) Serikali iendelee kutenga fedha za mishahara kwa wafanyakazi wa MSCL na iboreshe maslahi kwa watumishi;na

e) Serikali ihakikishe watumishi wazawa wanashirikishwa kikamilifu katika ujenzi wa miradi na ulinzi wa miundombinu;
f) MSCL ihakikishe ukarabati wa meli uende sambamba na ukarabati wa majengo na miundombinu ya Bandari;
g) Serikali ilitekeleze ahadi ya kujenga Meli mpya ziwa Tanganyika ili kutoa huduma kwa wananchi;
h) Mchakato wa TPA kuzikabidhi Meli zilizopo Ziwa Nyasa kwa MSCL ukamilike haraka;
i) Baada ya ukarabati wa Meli kukamilika TRC na TPA washirikiane ili kushika soko la usafirishaji wa mizigo;
j) Serikali ikarabati Barabara ya kutoka na kuingia Bandari ya Mwanza Kaskazini kwani wateja wameikimbia bandari hiyo kutokana na kutopitika;
k) Serikali ikarabati meli ya MV Liemba ili kunusuru maisha ya watu, katika ziwa Tanganyika; na
l) MV Mwongozo ifanyiwe uhakiki kikamilfu na wataalamu ili kujiridhisha kama inafaa kuendelea kutumika.

**3.4.2 Mheshimiwa Spika**, Kuhusu ATCL, TAA na TCAA Kamati inashauri kwamba;

a) Serikali isimamie ATCL ilipwe madeni yake ili yaweze kuweka sawa mizania ya shirika;
b) Serikali ishirikiane na ATCL, TAA na TCAA kupunguza gharama za usafiri wa ndani wa Ndege kwani gharama hizo ni kubwa;

c) Serikali ihakikishe miradi yote ya ujenzi wa viwanja vya ndege inakuwa chini ya TAA;
d) ATCL ione uwezekano wa kuongeza idadi ya safari za Ndege kubwa kwa siku zenye mahitaji makubwa ya abiria kati ya Dar es Salaam na Dodoma; na
e) ATCL iondoe mawakala ambao wamebainika kuwa wanahujumu Shirika kwa kutoa taarifa kwa wateja kuwa ndege imejaa wakati hali halisi ndege iko tupu.

**3.4.3 Mheshimiwa Spika,** kuhusu LATRA Kamati inashauri kwamba, LATRA ichukue hatua kwa baadhi ya mabasi ambayo yamebainika kwenda mwendo zaidi ya ule unaoruhusiwa wa kilomita 80 kwa saa.

**3.4.4 Mheshimiwa Spika,** kuhusu TMA Kamati inashauri kwamba:-
a) Serikali iboreshe maslahi ya wataalamu wa Mamlaka hii kwani wapo ambao wanahamia taasisi nyingine za ndani na nje ya nchi kutafuta maslahi bora; na
b) Serikali iisaidie TMA ili iweze kulipwa madeni yake wanayodai Taasisi za Serikali.

**3.4.5 Mheshimiwa Spika,** kuhusu TAZARA Kamati inashauri kwamba:-
a) Serikali ihakikishe mashine ya kuponda kokoto iliyopo TAZARA Mbeya inafanya kazi ipasavyo;
b) TAZARA ihakikishe mabehewa yanayohitaji ukarabati yanakarabatiwa ili yaendelee kutumika; na
c) Serikali iharakishe marekebisho ya Sheria ya TAZARA ili kuongeza ufanisi.

# SEHEMU YA NNE

# 4.0 HITIMISHO

## 4.1 Maelezo ya Kuhitimisha

**Mheshimiwa Spika**, sekta ya Ujenzi na Uchukuzi ni muhimu katika ukuaji wa uchumi wa nchi kwani sekta hizi huwezesha sekta nyingine zote kuweza kufikia malengo. Uwekezaji wake ni chachu ya maendeleo ya uchumi na kijamii katika kufanikisha Malengo ya Maendeleo Endelevu *(SDGs)* katika uimarishaji wa viwanda, ubunifu na miundombinu (kama inavyoeleza katika lengo Na. 9).

## 4.2 Shukrani na Wasilisho

**Mheshimiwa Spika,** kwa niaba ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu, naomba kumshukuru kwa dhati Mhe. Prof. Makame Mnyaa Mbarawa (Mb), Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi akishirikiana na Manaibu Mawaziri Mhe. Eng. Msongwe Geofrey Kasekenya (Mb) (Ujenzi), na Mhe. Atupele Fredy Mwakibete (Mb) (Uchukuzi) kwa ushirikiano mzuri wanaoutoa kwa Kamati.

**Mheshimiwa Spika,** nawashukuru pia Makatibu Wakuu, Naibu Makatibu Wakuu na Watendaji wote wa Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, kwa kuwawezesha Mawaziri na Naibu Mawaziri kutoa ushirikiano kwa Kamati.

**Mheshimiwa Spika**, nitumie fursa hii kumshukuru Katibu wa Bunge Ndugu Nenelwa Joyce Mwihambi kwa kuiwezesha Kamati wakati wote ilipokuwa inatekeleza majukumu yake. Aidha, shukrani maalumu ziende kwa Sekretarieti ya Kamati ikiongozwa na Mkurugenzi wa Kamati za Bunge ndugu Athuman Hussein, Mkurugenzi Msaidizi Gerald Singano Magili pamoja na Makatibu wa Kamati ndugu Janeth Julian Malangu, ndugu Victory Eliekimu Mrema na Msaidizi wa Kamati ndugu Grace Samwel Gwivaha pamoja na wafanyakazi wote wa Ofisi ya Bunge kwa ushirikiano wao ulioiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake ipasavyo.

**Mheshimiwa Spika**, aidha, napenda kuwashukuru wajumbe wa Kamati kwa ushirikiano na michango waliyoitoa wakati wa kupitia na kuchambua Bajeti pamoja na kuandaa taarifa hii. Naomba kuwatambua Wajumbe wa Kamati hii kwa kuwataja majina kama ifuatavyo: -

1. Mhe. Moshi Seleman Kakoso, Mb - Mwenyekiti
2. Mhe. Anne Kilango Malecela, Mb - M/Mwenyekiti
3. Mhe. Ahmed Mabkhut Shabiby, Mb - Mjumbe
4. Mhe. Zuberi Mohamed Kuchauka, Mb ″
5. Mhe. Capt. Abbas Ali Hassan Mwinyi, Mb ″
6. Mhe. Miraji Jumanne Mtaturu, Mb ″
7. Mhe. Fredrick Edward Lowassa, Mb ″
8. Mhe. Eng. Mwanaisha Ng'anzi Ulenge, Mb ″
9. Mhe. Mohamed Maulid Ali, Mb ″

10. Mhe. Innocent Edward Kalogeris, Mb ″
11. Mhe. Mbarouk Juma Khatibu, Mb ″
12. Mhe. Masache Njelu Kasaka, Mb ″
13. Mhe. Ahmed Ally Salum, Mb ″
14. Mhe. Amina Ally Mzee, Mb ″
15. Mhe. Rose Vicent Busiga, Mb ″
16. Mhe. Ally Anyigulile Jumbe Mlaghila, Mb ″
17. Mhe. Sophia Hebron Mwakagenda, Mb ″
18. Mhe. Stella Simon Fiyao, Mb ″
19. Mhe. Aeshi Khalfan Hilaly, Mb ″
20. Mhe. Abdulaziz M. Abood, Mb ″
21. Mhe. Innocent Sebba Bilakwate, Mb ″
22. Mhe. Ghati Zephania Chomete, Mb ″
23. Mhe. Ahmed Yahya Abdulwakil, Mb ″
24. Mhe. Bahati Khamis Kombo, Mb ″
25. Mhe. Angelina Malembeka, Mb ″

**Mheshimiwa Spika,** baada ya maelezo hayo naliomba Bunge lako lipokee, lijadili na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi kwa mwaka wa fedha 2022/2023 kama ilivyowasilishwa na mtoa hoja muda mfupi uliopita.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja.

Moshi Seleman Kakoso, Mb

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU**

**YA BUNGE YA MIUNDOMBINU**

23 Mei, 2022

## Kiambatisho Na.1

## Makusanyo ya Taasisi ya uchukuzi

| Na. | JINA LA TAASISI | MAKADIRIO YA MAKUSANYO KWA 2021/2022 | MAKADIRIO YA MAKUSANYO KWA 2022/2023 |
|---|---|---|---|
| | **Uchukuzi** | | |
| 1. | NIT | Bil. 24.2 | Bil. 26.1 |
| 2. | SNOTASHIP | Bil.15.48 | Bil.17.03 |
| 3. | TAZARA | Bil. 121 | Bil.123 |
| 4. | KADCO | Bil.7.6 | Bil. 19.08 |
| 5. | TAA | Bil.35.4 | Mil.226.40 |
| 6. | TRC | Bil. 29.20 | - |
| 7. | MSCL | Bil. 3.37 | - |
| 8. | TCAA | - | Bil. 3.5 |